



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**



**MWONGOZO WA UPIMAJI SHIRIKISHI WA**

**MATOKEO YA UJIFUNZAJI**

**KWA WATHIBITI UBORA WA SHULE**

**2023**





© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Toleo la Kwanza, 2023.

ISBN: 978-9987-09-547-6

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,  
Mji wa Serikali - Mtumba,  
Mtaa wa Afya,  
S.L.P 10,  
**40479 Dodoma.**

Simu: +255 26 296 3533

Baruapepe: [info@moe.go.tz](mailto:info@moe.go.tz)

Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

Mwongozo huu utarejelewa kama:

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). Mwongozo wa Upimaji Shirikishi wa Matokeo ya Ujifunzaji kwa Wathibiti Ubora wa Shule (UShiMU) - DPLA. Dodoma.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kurudufu, kupiga chapa, wala kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.





## Yaliyomo

<b>Shukurani</b> .....	v
<b>Vifupisho Vya Maneno</b> .....	vii
<b>SEHEMU YA KWANZA</b> .....	1
<b>UTANGULIZI</b> .....	1
1.1 Usuli.....	1
2.2 Lengo La Mwongozo.....	3
3.3 Umuhimu Wa Upimaji.....	4
4.4 Muundo Wa Mwongozo.....	5
5.5 Walengwa Wa Mwongozo.....	5
6.6 Wanufaika.....	5
<b>SEHEMU YA PILI</b> .....	6
<b>UTEKELEZAJI WA UPIMAJI WA MATOKEO YA UJIFUNZAJI</b> .....	6
2.1 <b>UTANGULIZI</b> .....	6
2.1.1 <b>UPIMAJI KATIKA ELIMU YA AWALI</b> .....	6
2.1.1 <b>UPIMAJI WA MATOKEO YA UJIFUNZAJI KATIKA DARASA LA I NA II</b> .....	15
<b>SEHEMU YA TATU</b> .....	25





WATENDAJI NA MAJUKUMU YAO KATIKA	
KUTEKELEZA UPIMAJI.....	25
3.1 UTANGULIZI.....	25
<b>SEHEMU YA NNE</b> .....	28
ZIARA YA UTHIBITI UBORA WA SHULE.....	28
4.1 UTANGULIZI.....	28
5.2 ZANA ZA TATHMINI ZA UBORA WA SHULE.....	28
6.3 MATAYARISHO KABLA YA ZIARA.....	29
7.4 ZIARA SHULENI.....	30
8.5 UANDISHI WA TAARIFA.....	31
<b>SEHEMU YA TANO</b> .....	32
URATIBU NA USIMAMIZI.....	32
5.1 UTANGULIZI.....	32
6.2 MAHITAJI NA VITENDEA KAZI.....	32
7.3 UWASILISHAJI WA TAARIFA NA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU.....	32
8.4 UFUATILIAJI NA TATHMINI.....	33
5.5 TATHMINI YA VIWANGO VYA UBORA KATIKA ELIMU YA AWALI, DARASA LA I NA II.....	34
VIASHIRIA NA VIGezo - UShiMU (DPLA).....	38
<b>Marejeleo</b> .....	43





## Shukurani

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) inatoa shukurani kwa wadau wote walioshiriki katika uandishi wa Mwongozo wa Upimaji Shirikishi wa Matokeo ya Ujifunzaji kwa Wathibiti Ubora wa Shule (UShiMU) - DPLA.

Shukurani hizi zinatolewa kwa wataalamu wathibiti ubora wa shule wafuatao ambao wameshiriki kwenye uandaaji wa Mwongozo huu, wakiwamo Lujeko Mwinuka, Raymond Mangulu, Hawa Selemani, na Norbet Mpunga kutoka WyEST, Hamis Mbinga (Newala), Verena Nchimbi na Nuru Mwevira (Morogoro), Consolata Mbogolo, Mwaluke Luhambati na Yoge Mwakawago (Nyanda za juu Kusini), Thomas Lima (Ruvuma), Mw Bakari Sagini (OR- TAMISEMI), Riaz Abeid (OR- TAMISEMI), Jackson Mpankuli .

WyEST pia, inatoa shukurani kwa wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni Dkt. Fortunatha Pembe, Dkt. Rose Ephraim, na Dkt. Johaiven Kashaigili waliokuwa wataalamu waelekezi katika kufanikisha uandishi wa mwongozo huu.

Vilevile, shukurani zinatolewa kwa wathibiti ubora wa shule kutoka WyEST, kanda na wilaya, ikiwamo kanda ya kati, kanda ya Dar es Salaam, nyanda za juu kusini pamoja na Wilaya ya Temeke, Ubungo, Kisarawe, Lushoto, Igunga,



Sikonge, Kilolo, Gairo na Manispaa ya Morogoro.  
WyEST inatoa shukurani za pekee kwa wafuatao:

**Wahariri:** Maimuna Amour kutoka WyEST  
Dkt. Maryam Mwinyi kutoka WyEST  
Dkt. Rehema Ogha Stephano kutoka chuo  
kikuu cha Dododma  
Hawa Selemani kutoka WyEST  
Noreen Kwezi kutoka chuo cha ualimu  
Nachingwea  
Musa Swira kutoka chuo cha ualimu  
Mhonda

**Wataalamu waelekezi:** Dkt. Jonathan Stern kutoka RTI  
Marekani  
Pilli Mazege kutoka WyEST  
Venance N. Manori kutoka WyEST

**Mratibu:** Hawa Selemani kutoka WyEST

**Msanifu:** Peter Mbute

Mwisho, shukurani za dhati zinatolewa kwa Shirika la  
Msaada wa Watu wa Marekani (USAID) kupitia Mradi wa  
Tusome Pamoja na Tujifunze Uelewa, kwa msaada wa  
kitaalamu na ufadhili uliofanikisha mchakato wa uandishi  
wa mwongozo huu.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**Kamishna wa Elimu,**

**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**



## Vifupisho vya Maneno

<b>DPLA</b>	Decentralization Periodic of Learning Assessment
<b>ESDP</b>	Education Sector Development Program
<b>GALA</b>	Group Administer of Learning Assessment
<b>IUUS</b>	Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule
<b>JzK</b>	Jumuiya za kujifunza
<b>KKK</b>	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
<b>KS</b>	Kamati ya Shule
<b>KUUS</b>	Kiunzi wa Wathibiti Ubora wa Shule
<b>KUMUVEA</b>	Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali
<b>LQAS</b>	Lot Quality Assurance Sampling
<b>MKUUS</b>	Mpango wa Kuboresha Utendaji Shuleni
<b>MUUS</b>	Mpango wa Uthibiti Ubora wa Shule
<b>MUVEA</b>	Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali
<b>OAEM</b>	Ofisi ya Afisa Elimu Msingi





<b>OR -</b>	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali
<b>TAMISEMI</b>	za Mitaa
<b>TEHAMA</b>	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
<b>TWUS</b>	Timu ya Wathibiti Ubora wa Shule
<b>UShiMU</b>	Upimaji Shirikishi wa Matokeo ya Ujifunzaji.
<b>URT</b>	United Republic of Tanzania
<b>UUS</b>	Uthibiti Ubora wa Shule
<b>UUSW</b>	Uthibiti Ubora wa Shule Wilaya
<b>UWaWa</b>	Ushirikiano wa Wazazi na Walimu
<b>WyEST</b>	Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia







# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 USULI

Utoaji wa elimu bora nchini ni muhimu kwa maendeleo ya taifa. Suala la upimaji wa mara kwa mara wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi shuleni ni shirikishi na ni ajenda ya kitaifa katika kufikia lengo la utoaji wa elimu bora. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Dira ya elimu nchini vinasisitiza kuwa na mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo, na mtazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya taifa (URT, 2014). Katika kufikia lengo hilo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) azma ya kuinua ubora wa elimu na mafunzo ili kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.

Katika kutafsiri Sera hiyo ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Wizara imeweka mikakati yake kwenye Mpango wa Ki - Sekta wa Maendeleo ya Elimu wa miaka mitano (Education Sector Development Program - ESDP) (2020/2021 - 2025/2026). Mpango wa Maendeleo ya Elimu nchini unasisitiza katika kupima matokeo ya





ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi kuanzia Elimu ya Awali mpaka Sekondari. Mpango huu umebainisha umuhimu wa kuongeza jitihada za kuinua kiwango cha ubora wa elimu katika ngazi zote. Lengo ni kutekeleza na kuhakikisha kuwa mtoto/mwanafunzi anapata mafanikio katika ujifunzaji pamoja na umahiri uliokusudiwa kutokana na maarifa, stadi na mwelekeo chanya utakaomwezesha kuwa na makuzi timilifu kuweza kuchangia maendeleo ya taifa.

Ili kufikia lengo hilo WyEST kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule (IUUS), ina wajibu wa kufanya tathmini ya ubora wa utoaji wa elimu nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa elimu itolewayo nchini inakidhi mahitaji ya ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi ili kufikia viwango vya kikanda na kimataifa. WyEST, kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, iliandaa Kiunzi cha Kitaifa kinachotoa dira katika kuangalia na kutathmini viwango vya ubora wa elimu itolewayo. Kiunzi hicho kinasisitiza suala la ufundishaji unaokidhi ujifunzaji na upimaji mzuri wa matokeo ya mtoto/mwanafunzi. Hivyo, tathmini ya ubora wa elimu itolewayo kwa kuzingatia ubora wa matokeo ya ujifunzaji inafanywa kwa kutumia nyanja sita ambazo ni:

- i. Mafanikio ya wanafunzi;
- ii. Ubora wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji mzuri;
- iii. Ubora wa mtaala katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi;





- iv. Ubora wa uongozi na utawala: uongozi wa ujifunzaji, uongozi wa watu na rasilimali nyingine;
- v. Ubora wa mazingira ya shule na athari zake kwenye ustawi, afya na usalama; na
- vi. Ushiriki wa Jamii.

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa stadi za awali za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika Elimu ya Msingi umepewa kipaumbele ili kupata matokeo ya ujifunzaji katika uwanja wa kwanza kwenye Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule (KUUS). Hata hivyo, vigezo vya kupima matokeo ya ujifunzaji wa mwanafunzi katika uwanja huo havikuandaliwa sambamba na Kiunzi. Hivyo, mwongozo huu unatoa maelekezo ya namna ya kupima matokeo ya ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi ili kupata taarifa stahiki katika uwanja wa mafanikio ya mtoto/mwanafunzi na kutunza kumbukumbu. Vilevile, mwongozo huu unatoa maelekezo yanayobainisha namna Wathibiti Ubora wa Shule (WUS) watakavyotekeleza majukumu yao katika kupima na kutathmini matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji ili kutoa mrejesho kwa wadau wote kuanzia ngazi ya shule hadi ngazi ya taifa.

## 1.2 LENGU LA MWONGOZO

Lengu la mwongozo huu ni kutoa maelekezo stahiki kwa wathibiti ubora wa shule, maafisa elimu, na walimu, kuhusu





upimaji na tathmini ya matokeo ya ujifunzaji kwa mtoto wa Elimu ya Awali na mwanafunzi wa darasa la I na II.

### **1.3 UMUHIMU WA UPIMAJI**

Uzoefu uliopatikana kwa miaka mitatu katika mikoa ya Iringa, Morogoro, Mtwara, na Ruvuma kuanzia mwaka 2016 hadi 2018, kupitia mradi wa TUSOME PAMOJA kwa kushirikiana na WyEST, unaonesha kuwa matokeo ya ujifunzaji wa stadi za KKK kwa wanafunzi wa darasa la pili, yanaweza kupimwa kwa kutumia mfumo shirikishi baina ya wathibiti wbora wa shule, viongozi na wadau mbalimbali katika ngazi ya halmashauri, unaoitwa upimaji shirikishi wa matokeo ya ujifunzaji (UShiMU).

Aidha, upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi kwa kutumia mfumo shirikishi, unatoa fursa kwa wadau wa elimu katika ngazi husika ya halmashauri kupata taarifa kuhusu maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji katika shule zao na kuweza kuweka mikakati ya pamoja ya namna ya kutatua changamoto zilizoibuliwa kwenye upimaji.

Kwa hiyo, mwongozo huu unatoa maelekezo kwa watekelezaji wa mfumo huu wa upimaji ili kuimarisha upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi.





## **1.4 MUUNDO WA MWONGOZO**

Mwongozo huu una sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wenye usuli, lengo la Mwongozo, umuhimu wa upimaji, muundo, walengwa na wanufaika wa Mwongozo. Sehemu ya pili inaelezea namna ya kutekeleza upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto/mwanafunzi, wajibu na majukumu ya watendaji katika kila ngazi. Sehemu ya tatu inahusu ziara za Uthibiti Ubora wa Shule (UUS). Sehemu ya nne inaelezea uratibu na usimamizi. Sehemu ya tano inaelezea viashiria na vigezo vya upimaji wa matokeo ya mwanafunzi.

## **1.5 WALENGWA WA MWONGOZO**

Watumiaji wa mwongozo huu ni wakurugenzi wa halmashauri, wathibiti ubora wa shule ngazi zote, maafisa elimu ngazi zote, wakuu wa shule, walimu, na wadau wengine wa elimu.

## **1.6 WANUFAIKA**

Wanufaika wa mwongozo huu ni watoto/wanafunzi wa Elimu ya Awali, darasa la I, la II, na walimu wa madarasa hayo.





## SEHEMU YA PILI

# UTEKELEZAJI WA UPIMAJI WA MATOKEO YA UJIFUNZAJI

### 2.1 UTANGULIZI

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji utafanyika kuanzia Elimu ya Awali mpaka ya Msingi darasa la I na II kwa kuzingatia vigezo na viashiria pendekezwa.

#### 2.1.1 UPIMAJI KATIKA ELIMU YA AWALI

Upimaji unaangalia uwezo anaotakiwa kujengewa mtoto katika nyanja zote za ukuaji na ujifunzaji kiakili, kimwili, kijamii, na kihisia kupitia vitendo mbalimbali vya ujifunzaji. Upimaji utafuata hatua kuu tatu ambazo ni maandalizi, ukusanyaji wa taarifa za upimaji wa matokeo ya ujifunzaji, na uchakataji wa taarifa za matokeo ya upimaji na uandishi wa taarifa.

##### 2.1.1.1 Maandalizi ya Upimaji katika Elimu ya Awali

Hatua hii itahusisha kupata idadi ya sampuli za shule na watoto pamoja na ratiba ya kutembelea shule hizo.

##### i. Upatikanaji wa Sampuli za Shule

Madarasa ya Elimu ya Awali na Shule za





Msingi zitahusika katika kupata sampuli. Kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, idadi ya shule kumi na tisa (19) zitahusika katika upimaji. Idadi hiyo ya shule 19 itapatikana kwa kutumia uchaguzi nasibu (random sampling) katika kila halmashauri. Shule hizi zitachaguliwa kutoka kwenye shule ambazo tayari ziko kwenye mpango wa kutekeleza tathmini ya jumla ya shule.

## **ii. Upatikanaji wa Sampuli ya Watoto**

Watoto 21 watachaguliwa kwa kutumia uchaguzi nasibu kutoka kila shule iliyochaguliwa kushiriki zoezi la upimaji. Kati ya watoto hao 21, watoto 19 watapimwa na 02 watabaki kuwa wa ziada ili kuchukua nafasi endapo wengine hawatapenda kushiriki katika zoezi hilo.

## **iii. Ratiba ya Kutembelea Shule**

Baada ya shule kuteuliwa, wathibiti ubora wa shule wataandaa ratiba ya zoezi la upimaji wa siku moja kwa kila shule.





### **2.1.1.2 Kukusanya Taarifa za Upimaji wa Matokeo ya Ujifunzaji**

Hatua hii itahusisha kukusanya taarifa za upimaji wa matokeo ya ujifunzaji. Mchakato wa kupima matokeo ya ujifunzaji utakuwa shirikishi utakaowahusisha wathibiti ubora wa shule, maafisa elimu, wakuu wa shule, na walimu wa darasa la awali. Mambo muhimu ya kuzingatia katika hatua hii ni haya yafuatayo:

#### **i. Maandalizi ya Kufanya Upimaji**

Kabla ya kuanza upimaji wa matokeo ya ujifunzaji, ni lazima maandalizi ya upimaji wa mtoto yafanyike. Hii itasaidia kujua utayari wake kwa ajili ya zoezi la upimaji kabla ya kuanza upimaji wenyewe. Vifaa vya upimaji, vikiwamo vichocheo vya vitendo changamshi vya mtoto, suhula za kufanyia uchangamshi, orodha hakiki, na mkoba wa kazi vitatumika katika upimaji. Mpimaji, kama siyo mwalimu wa shule husika, atalazimika kuomba ridhaa kutoka mamlaka husika kabla ya kufanya zoezi hilo (rejea Kiongozi cha Ufundishaji wa Elimu ya Awali kinachotumika na vitabu vya rejea katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto).







## ii. Mazingira ya Kufanyia Upimaji

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unatakiwa ufanyike katika mazingira tulivu yanayoruhusu ujifunzaji. Kabla ya kuanza kupima, mpimaji ahakikishe kuwa mazingira ni salama, tulivu, na hakuna mwingiliano wa watu na vitu ambavyo vinaweza kusababisha mtoto asiwe na usikivu. Aidha, mpimaji atatakiwa kujenga mazingira ya kirafiki na mtoto kwa kumuuliza maswali kuhusu michezo anayopenda kucheza au kitu kingine kinachomfurahisha katika mazingira aliyopo. Mpimaji ajitahidi kuweka ukaribu na mtoto ili mtoto aone kwamba kinachoendelea kufanyika ni vitendo vya michezo na si mtihani.

### 2.1.1.3 Mambo Muhimu ya Kuzingatia katika Upimaji

Ili upimaji ufanyike kwa ufanisi, yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia:

- a. Lengo la upimaji;
- b. Mtaala wa Elimu ya Awali;
- c. Muhtasari wa Elimu ya Awali;





- d. Mwongozo wa Mwalimu wa kufundishia Elimu ya Awali;
- e. Mahitaji ya mtoto;
- f. Zana za upimaji; na
- g. Muda wa upimaji.

#### **2.1.1.4 Umahiri Unaokusudiwa Kupimwa**

Upimaji utafanyika katika mahiri zote kulingana na Muhtasari wa Elimu ya Awali ambazo ni umahiri wa Kuhusiana, Kuwasiliana, Kutunza afya, Kutunza Mazingira, Kutumia Dhana za Kihisabati na Kumudu Stadi za Kisanii. Yafuatayo ni maelezo ya mahiri hizo:

##### **a. Umahiri wa Kuhusiana**

Umahiri huu unahusisha mabadiliko ya mtoto kitabia; kiuhusiano; utayari katika kutenda na kuiga; kushirikiana; kuthamini utu wake wa watu wengine na vitu vilivyoko katika mazingira; kuonesha uvumilivu; uzalendo na kuwa na mtazamo chanya (rejea Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango pamoja na Zana ya Upimaji wa Kumudu Stadi za Kuhusiana).





### **b. Umahiri wa Kuwasiliana**

Umahiri wa kuwasiliana humwezesha mtoto kukua kiakili, kijamii, na kihisia. (rejea Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango pamoja na Zana ya Upimaji wa Kumudu stadi za Kuwasiliana).

### **c. Umahiri wa Kutunza Afya**

Sehemu hii inalenga kumwezesha mtoto kujenga uwezo wa kutunza afya. Upimaji wa mtoto utahusisha mabadiliko yanayotokana na vitendo anavyofanya katika kubainisha sehemu za nje za mwili wa binadamu, kutumia vifaa vya kufanyia usafi wa mwili, mavazi na namna anavyoyatumia mazingira yake kujifunza (rejea Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango pamoja na Zana ya Upimaji wa Kumudu Stadi za Kutunza Afya).

### **d. Umahiri wa Kutunza Mazingira**

Umahiri wa kutunza mazingira utamwezesha mtoto kuyapenda, kuyajali, kuyathamini pamoja na kupata stadi za kutunza mazingira hayo (rejea Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji





na Viwango pamoja na Zana ya Upimaji wa Kumuda Stadi za Kutunza Mazingira).

**e. Umahiri wa Kumudu Stadi za Kisanii**

Umahiri huu utamwezesha mtoto kuwa na stadi za ubunifu kwa kuzingatia ujumi unaojitokeza ili kuleta uhalisia (rejea Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango pamoja na Zana ya Upimaji wa Kumudu Stadi za Kisanii).

**f. Umahiri wa Kutumia Dhana za Kihisabati**

Umahiri huu utamwezesha mtoto kufikiri, kutenda, na kutumia dhana za Kihisabati na TEHAMA katika maisha ya kila siku (rejea Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango pamoja na Zana ya Upimaji wa Kumudu Stadi za Kutumia Dhana za Kihisabati).

**2.1.1.5 Zana za Tathmini ya Ubora wa Shule**

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji utafanyika kwa kutumia zana stahiki ambazo ni:

- i. Fomu ya tathmini binafsi ya shule;
- ii. Tathmini binafsi ya mwalimu;





- iii. Fomu ya uchunguzi darasani;
- iv. Zana ya kichocheo cha michezo;
- v. Fomu ya Makuzi na Maendeleo ya Mtoto;
- vi. Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali (MUVEA); na
- vii. Kiongozi cha Utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji na Viwango katika Elimu ya Awali.

**a. Wakati wa Upimaji**

Mpimaji amwelekeze mtoto namna ya kuanza kucheza, amwoneshe tabasamu, na amweleze nini cha kufanya. Aanze kutambulisha mchezo na kufuata maelekezo hatua kwa hatua. Asome vizuri maelekezo katika Mwongozo wa mpimaji, kisha ampe mtoto kichocheo cha michezo kinachoonesha vitendo vya michezo iliyopendekezwa. Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji wa mtoto umegawanyika katika makundi matatu, yakijumuisha upimaji wa awali, endelevu na tamati.

**b. Namna ya Kupima Viwango vya Utendaji**  
Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unatakiwa





kuzingatia viashiria vya utendaji ili kupata matokeo tarajiwa. Alama ya vema ( $\surd$ ) itawekwa mara baada ya kupima matokeo ya utendaji kwa njia ya mchezo aliouchagua mpimaji. Ifikapo mwisho wa upimaji, itamlazimu mpimaji kutenga muda kuhakikisha kuwa kila swali limewekewa alama ili kujumlisha alama zote na kupata takwimu sahihi. Jumla ya alama hizo zigawanywe kwa idadi ya maswali ili kupata wastani. Mpimaji azingatie viwango vya utendaji vilivyofikiwa katika umahiri husika kama ifuatavyo:

- i. Hajaweza* inamaanisha kuwa mtoto hajaonesha kumudu stadi iliyokuwa inapimwa;
- II. Wastani* inamaanisha kuwa mtoto amejaribu kwa kiasi kidogo kuonesha kumudu stadi iliyokuwa inapimwa;
- III. Vizuri* inamaanisha kuwa mtoto ameonesha kumudu stadi iliyokuwa inapimwa kwa kiwango cha kati; na
- IV. Vizuri sana* inamaanisha kuwa mtoto ameonesha kumudu stadi iliyokuwa inapimwa kwa kiwango cha juu.





Ili kuvitumia viwango hivi vizuri na kwa ufanisi, zana ya upimaji kwa kila umahiri itatumika ipasavyo kubaini viashiria vya utendaji kwa kila swali katika kichocheo cha mchezo.

**a. Kuchakata Taarifa za Matokeo ya Upimaji**

Utoaji taarifa za matokeo ya ujifunzaji wa mtoto utakuwa shirikishi ambapo mfumo wa mawasiliano ufuata utaratibu uliowekwa. Taarifa za maendeleo ya mtoto shuleni zitunzwe kwenye Kanzidata ya shule.

**b. Mrejesho wa Matokeo ya Upimaji**

Ni muhimu kwa mpimaji kutoa mrejesho wa matokeo ya upimaji. Kila ngazi ya utendaji ipate taarifa husika na kufanya maamuzi kutokana na changamoto itakayojitokeza ili kumwezesha mtoto kupata elimu bora.

## **2.1.2 UPIMAJI WA MATOKEO YA UJIFUNZAJI KATIKA DARASA LA I NA II**

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji katika darasa la I na II utatumia sauti za herufi, maneno ya kubuni, kusoma kwa ufahamu, imla na umahiri wa kuhesabu. Lengo la upimaji huu ni kubaini kiwango cha ujifunzaji wa mwanafunzi na stadi zilizoibuliwa wakati wa ujifunzaji. Upimaji huu





huzingatia mambo ambayo mwanafunzi amejifunza, uzoefu wake, mahitaji yake, na umahiri anaojifunza. Uwezo wa mwanafunzi unaangaliwa sana katika kujifunza umahiri wa Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (KKK). Kiwango cha utendaji kilichofikiwa kitategemea zaidi alama zitakazopatikana katika umahiri wa KKK.

### **2.1.2.1 Namna ya Kupima Viwango vya Utendaji**

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unatakiwa kuzingatia viashiria vya utendaji ili kuona kama vimefikiwa au havijafikiwa. Uainishaji huu unasaidia watendaji wa ngazi zote kuelekeza msaada wao kwenye shule au wilaya zenye uhitaji zaidi. Viashiria vinavyotumika katika upimaji ni pamoja na:

#### **i. Mahitaji ya Shule**

- a. Mahudhurio ya walimu;
- b. Mahudhurio ya wanafunzi;
- c. Kamati ya Shule;
- d. Taarifa za usajili wa watoto;
- e. Muda wa kufanya kazi;
- f. Upatikanaji wa vifaa vya kufundishia; na
- g. Upatikanaji wa vifaa vya wanafunzi.







## ii. Utendaji wa Mwalimu

- a. Ushiriki wa wanafunzi;
- b. Muda wa kufundisha umahiri;
- c. Mazoezi ya umahiri wa Kusoma;
- d. Utayari wa mwalimu;
- e. Mazingira rafiki na salama;
- f. Elimu jumuishi;
- g. Uwapo wa daftari kwa kila mwanafunzi;  
na
- h. Mrejesho wa mwalimu.

## iii. Matokeo ya Ujifunzaji

- a. Sauti za herufi;
- b. Maneno yasiyo na maana;
- c. Ufahamu;
- d. Imla;
- e. Utambuzi wa namba;
- f. Kujumlisha na kutoa ngazi ya kwanza;
- g. Kujumlisha na kutoa ngazi ya pili; na
- h. Namba inayokosekana katika mfuatano.

Viashiria hivi vinagawanyika katika nyanja sita zilizomo katika Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule kama ifuatavyo:





### **Uwanja wa Kwanza: Mafanikio ya Wanafunzi**

Viashiria vinavyohusika ni: matokeo ya wanafunzi katika kumudu umahiri wa Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu.

### **Uwanja wa Pili: Ubora wa Ufundishaji, Ujifunzaji na Upimaji Mzuri**

Viashiria vinavyohusika ni: ushiriki wa wanafunzi kwenye umahiri wa KKK, mazoezi ya umahiri wa kusoma, utayari wa mwalimu, Elimu Jumuishi, muda wa kufundisha umahiri, mrejesho wa mwalimu, sauti za herufi, maneno yasiyo na maana, ufahamu, imla, utambuzi wa namba, kujumlisha na kutoa ngazi ya kwanza, kujumlisha na kutoa ngazi ya pili, na namba inayokosekana katika mfuatano.

### **Uwanja wa Tatu: Ubora wa Mtaala katika Kukidhi Mahitaji ya Wanafunzi**

Viashiria vinavyohusika ni: upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika umahiri wa KKK.

### **Uwanja wa Nne: Ubora wa Uongozi na Utawala; Uongozi wa Ujifunzaji, Uongozi wa Watu na Rasilimali nyingine**

Viashiria vinavyohusika ni: Taarifa za usajili wa watoto, mahudhurio ya walimu na wanafunzi na kamati za shule.





## **Uwanja wa Tano: Mazingira Rafiki na Salama**

Viashiria vinavyohusika ni mazingira rafiki na salama ya ujifunzaji, ikiwamo miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na lishe shuleni.

## **Uwanja wa Sita: Ushiriki wa Jamii**

Viashiria vinavyohusika ni uwapo wa vikao vya Ushirikiano wa Wazazi na Walimu (UWaWa), Jumuiya za Kujifunza (JzK), na ushiriki wa wazazi/walezi katika kutengeneza zana.

Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini katika nyanja sita kwa darasa la I na II yanatokana na matokeo ya Upimaji Shirikishiki wa Matokeo ya Ujifunzaji (UShiMU) kwa kutumia Kifaa cha shule cha UShiMU - DPLA na kifaa cha Upimaji wa Usomaji na Hesabu kwenye kikundi - GALA (rejea vifaa vya UShiMU - DPLA).

### **2.1.1.2 Maandalizi ya Kufanya Upimaji**

Kabla ya kuanza upimaji wa matokeo ya ujifunzaji, mpimaji anapaswa kufanya maandalizi ya vifaa vya upimaji, vikiwamo vifaa vya shule kwa ajili ya kupata taarifa kutoka kwa mkuu wa shule, fomu ya matokeo katika shule; kadi za namba na chati ya namba ya uteuzi wa wanafunzi; fomu za upimaji wa usomaji na upimaji wa hesabu kwenye kikundi A na B



(GALA); penseli, vifutio na vichongeο (rejea orodha ya vifaa vya upimaji UShiMU - DPLA).

### **2.1.2.3 Mazingira ya Kufanyia Upimaji**

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji unatakiwa kufanyika katika mazingira tulivu yanayoruhusu ujifunzaji. Kabla ya kuanza kupima, mpimaji ahakikishe kuwa mazingira ni salama na tulivu, na hakuna mwingiliano wa watu na vitu ambavyo vinaweza kusababisha mwanafunzi asiwe na usikivu. Aidha, anatakiwa kujenga mazingira ya kirafiki kwa mwanafunzi ili atambue kwamba kinachoendelea kufanyika ni zoezi na siyo mtihani.

### **2.1.2.4 Mambo Muhimu ya Kuzingatia katika Upimaji**

Ili upimaji ufanyike kwa ufanisi, yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia:

- i. Lengo la upimaji;
- ii. Mtaala wa Darasa la I na II;
- iii. Mwongozo wa mwalimu wa kufundishia Darasa la I na II;
- iv. Mahitaji ya mwanafunzi kwa kuzingatia Elimu Jumuishi;



- v. Zana za upimaji;
- vi. Zana za ukusanyaji wa matokeo;
- vii. Vitabu vya umahiri wa KKK;
- viii. Vitabu vya ziada vya umahiri wa KKK; na
- ix. Muhtasari wa Elimumsingi Darasa la I na II.

Baada ya kumaliza uangalizi wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, mpimaji atatakiwa kujitambulisha, kuwaeleza wanafunzi lengo la zoezi la upimaji na jinsi utakavyofanyika, na namna ya kuwapata wanafunzi watakaoshiriki zoezi la upimaji. Aidha, atawaweka wanafunzi katika mduara/mstari kwa kuwachanganya wasichana na wavulana. Atagawa kadi za namba kwa wanafunzi wote, kisha atachagua wanafunzi 21 kwa kutumia uchaguzi nasibu. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 19 watapimwa na 02 watabaki kuwa wa ziada ili kuchukua nafasi endapo wengine hawatapenda kushiriki katika zoezi hilo. Mpimaji ataingia na wanafunzi husika darasani na atawapatia vifaa, vikiwamo penseli, vichongeο, vifutio, na karatasi za “GALA” A au B, mpimaji atatoa maelekezo ya awali kabla ya kuanza zoezi, kisha hatua za upimaji wa KKK zitaanza kwa kufuata maelekezo ya upimaji, na mwisho atakusanya karatasi zote.





### **2.1.2.5 Umahiri Unaokusudiwa Kupimwa**

Upimaji utafanyika katika mahiri tatu ambazo ni Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

#### **i. Umahiri wa Kusoma**

Umahiri huu utamwezesha mwanafunzi wa darasa la I na II katika kukuza lugha ya mazungumzo, utambuzi wa sauti, utambuzi wa sauti za herufi, kusoma kwa ufasaha, ufahamu wa kusoma na kusikiliza, pamoja na matumizi ya msamiati (rejea Muhtasari wa Elimumsingi Darasa la I na II).

#### **ii. Umahiri wa Kuandika**

Umahiri huu utamwezesha mwanafunzi wa darasa la I na II katika ujenzi wa stadi za kuandika, uumbaji wa herufi, matumizi ya kanuni za uandishi, ufasaha na ushikamani, uandishi wenye mfuatano sahihi wa matukio, uandishi wa mwandiko wa chapa, na uundaji wa maneno (rejea Muhtasari wa Elimumsingi Darasa la I na II).

#### **iii. Umahiri wa Kuhesabu**

Umahiri huu utamwezesha mwanafunzi wa darasa la I na II katika utambuzi wa namba, utambuzi wa uhusiano wa vitu na namba,





utambuzi wa vipimo, utambuzi wa maumbo, na kukusanya na kuorodhesha vitu (rejea Muhtasari wa Elimumsingi Darasa la I na II).

### **2.1.2.6 Uchambuzi wa Taarifa za Upimaji na Uwekaji wa Kumbukumbu**

Uchambuzi na namna ya kutunza kumbukumbu baada ya kukusanya taarifa za upimaji utafanyika kwa kufuata hatua zifuatazo:

- i. Ofisi ya Afisa Elimu Msingi (OAEM) na Ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule Wilaya kufanya kikao cha pamoja cha mawasilisho ya matokeo ya upimaji;
- ii. Kubainisha maeneo yaliyoonesha mafanikio na yenye changamoto, kisha kuchagua maeneo matatu yenye viashiria vyenye matokeo ya chini zaidi;
- iii. Kuunda Mpango wa Kuboresha Utendaji Shuleni (MKUUS);
- iv. Kuwasilisha matokeo ya Upimaji na MKUUS kwa Afisa Elimu Mkoa ili kupitia na kutoa mapendekezo;
- v. Ofisi ya Afisa Elimu Msingi Wilaya (AEMW), Wathibiti Ubora wa Shule Wilaya na wadau





- wa elimu kufanya kikao cha mawasilisho ya matokeo na MKUUS kwa ajili ya utekelezaji;
- vi. Kufanya ufuatiliaji na tathmini; na
  - vii. Taarifa za matokeo ya upimaji na MKUUS kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu WyEST na OR - TAMISEMI.

### **2.1.2.7 Zana za Upimaji**

Vifaa vya upimaji na ukusanyaji taarifa vitasimamiwa na Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na kupitiwa na kikosi kazi chenye wawakilishi kutoka WyEST na OR - TAMISEMI. Vifaa hivi vitafuata ngazi na mtiririko wa kifaa cha shule na GALA ambavyo vimekuwa vikipitiwa na kikosi kazi na kutumika kupima matokeo ya ujifunzaji ya mwanafuzi kwa muda wa miaka mitatu.







## SEHEMU YA TATU

# WATENDAJI NA MAJUKUMU YAO KATIKA KUTEKELEZA UPIMAJI

### 3.1 UTANGULIZI

Utekelezaji wa upimaji utahusisha kamati tendaji ya wizara, wathibiti ubora wa shule, maafisa elimu kutoka ofisi ya elimu msingi, maafisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu, na timu ya uthibiti ubora wa shule wa ndani. Yafuatayo ni majuku ya kila kundi:

**i. Kamati Tendaji ya Wizara (WyEST na OR-TAMISEMI)**

- a. Kuchagua wawezeshaji wakuu;
- b. Kubainisha sifa za wawezeshaji wakuu;
- c. Kupitia vifaa vya upimaji/kukusanyia taarifa;
- d. Kuweka vigezo vya upimaji;
- e. Kupitia viashiria; na
- f. Kutoa maelekezo ya namna ya kufanya upimaji na utatuzi wa changamoto.

**ii. Wathibiti Ubora wa Shule**

- a. Kukusanya taarifa za UShiMU kwenye shule 19;





- b. Kupima wanafunzi 19 waliochaguliwa katika kila shule zilizoteuliwa;
- c. Kutoa mrejesho wa awali kwa shule zilizoshiriki zoezi, ikishirikisha mkuu wa shule na mwalimu wa darasa aliyeshiriki zoezi;
- d. Kuchakata na kutayarisha taarifa za matokeo ya UShiMU;
- e. Kuwasilisha taarifa za matokeo na MKUUS kwenye ngazi husika; na
- f. Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji.

### **iii. Maafisa Elimu wa Halmashauri**

- a. Kuchambua na kutayarisha taarifa za matokeo ya UShiMU;
- b. Kutayarisha MKUUS;
- c. Kuwasilisha MKUUS kwa Maafisa Elimu Kata; na
- d. Kufuatilia utekelezaji wa MKUUS.

### **iv. Maafisa Elimu Kata**

- a. Kuwasilisha taarifa za MKUUS shuleni;
- b. Kufuatilia utendaji;
- c. Kutoa taarifa mara kwa mara kwa Maafisa Elimu wa Halmashauri kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa MKUUS; na





d. Kufuatilia utekelezaji wa MKUUS kwenye JzK, UWaWa, Kamati za Shule, na walimu.

**v. Wakuu wa Shule, Walimu, na Timu ya Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani**

- a. Kufuatilia utekelezaji wa MKUUS;
- b. Kutoa taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa MKUUS kwa ngazi mbalimbali za uongozi; na
- c. Kufuatilia utekelezaji wa MKUUS kwenye JzK, UWaWa, kamati za shule, na walimu.

**iv. Walimu wa KKK**

- a. Kutekeleza MKUUS darasani; na
- b. Kutunza na kutoa taarifa za ujifunzaji na upimaji wa wanafunzi wake kwa ngazi mbalimbali za uongozi.





## SEHEMU YA NNE

### ZIARA YA UTHIBITI UBORA WA SHULE

#### 4.1 UTANGULIZI

Ziara ya Wathibiti Ubora wa Shule itafanyika kwa siku mbili au tatu kulingana na ukubwa wa shule baada ya shule kujitathmini na kujaza fomu ya tathmini hiyo na kuiwasilisha katika Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule ya Wilaya.

#### 4.2 ZANA ZA TATHMINI ZA UBORA WA SHULE

Upimaji wa matokeo ya ujifunzaji utafanyika kwa kutumia zana stahiki ambazo ni:

- i. Fomu ya tathmini binafsi ya shule;
- ii. Fomu ya uangalizi wa ufundishaji na ujifunzaji darasani;
- iii. Fomu ya kukutana na mkuu wa shule;
- iv. Fomu ya kukutana na wazazi/jamii;
- v. Fomu ya kukutana na walimu; na
- vi. Fomu ya kukutana na wanafunzi.





### 4.3 MATAYARISHO KABLA YA ZIARA

Kiongozi wa timu ya maafisa UUS atajiandaa kwa kutumia taarifa iliyotolewa na shule ili:

- i. Kupata picha ya jumla ya utendaji wa karibuni wa shule na muktadha wake kama ilivyoelezwa kwenye fomu ya tathmini binafsi ya shule;
- ii. Kupitia na kuchambua Mpango Kazi na Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule na nyaraka zingine zinazohusika zilizotolewa na shule;
- iii. Kuandaa mpango wa kabla ya ziara na kuusambaza kwa wajumbe wengine ili:
  - a. Kukumbushia na kusesitiza umuhimu wa kuzingatia kanuni za maadili wakati wote na kuchukua taarifa kwa usahihi pamoja na kufuata itifaki na taratibu zilizokubalika;
  - b. Kugawa na kujadili majukumu ya kila mjumbe wa timu, kufuatana na sifa na uzoefu wa maafisa Uthibiti Ubora wa Shule (UUS);
  - c. Kukumbusha timu juu ya ufanyaji kazi ya tathimini;
  - d. Kusoma fomu ya mpango wa kabla ya ziara na kufanya rejea kwenye Mwongozo wa Uthibiti Ubora wa Shule (MUUS) ili kujiandaa na majukumu yao maalumu wakati wakiwa kwenye eneo la kazi.





#### 4.4 ZIARA SHULENI

Kiongozi wa timu ya UUS akutane na mkuu wa shule ili:

- i. Kutambulisha timu na kusudi la ziara;
- ii. Kutayarisha kikao na mkuu wa shule;
- iii. Kukubaliana kuhusu ratiba na utaratibu kwa ajili ya kuona ufundishaji darasani, mijadala ya vikundi vya wanafunzi, wazazi/walezi, walimu, na watumishi wengine;
- iv. Kupanga utaratibu wa kutoa mrejesho kwa uongozi wa shule na walimu kuhusiana na mambo yaliyobainika na maeneo yanayohitaji maboresho kupitia nyanja sita za Uthibiti Ubora wa Shule;
- v. Kupata taarifa za watumishi waliopo na wasiokuwapo kazini au masuala mengine ambayo timu itapaswa kuyafahamu; na
- vi. Kukutana na watumishi ili kutambulisha wajumbe wa timu ya UUS na kuwaeleza kusudi la ziara yao.

Timu ya Wathibiti Ubora wa Shule (TWUS) itajihusisha na shughuli za tathmini au ufuatiliaji ili kupata hali halisi ya namna shule inavyoendeshwa. Shughuli zifuatazo zitazingatiwa wakati wa tathmini au ufuatiliaji:

- i. Kushuhudia ufundishaji na ujifunzaji ndani na nje ya darasa;
- ii. Kuangalia usahihishaji wa kazi za wanafunzi (taarifa ya kupimika) na mapitio ya nyaraka zilizopo shuleni;





- iii. Majadiliano na wadau wa elimu kuhusu maendeleo ya shule katika kuboresha taaluma;
- iv. Katika siku za tathmini au ufuatiliaji, kiongozi wa timu atatoa mrejesho wa kila siku kwa mkuu wa shule kuhusu maendeleo ya kazi ya tathmini au ufuatiliaji; na
- v. Baada ya kufanya tathmini, timu ya Uathibiti Ubora wa Shule itakaa kikao kifupi cha kufanya maamuzi kwa kuzingatia ushahidi uliopatikana ili kutoa mrejesho kwa wadau wote wa elimu shuleni katika kikao cha mwisho.

#### **4.5 UANDISHI WA TAARIFA**

TWUS itaandaa taarifa ya tathmini au ufuatiliaji na kuituma/ kuisambaza kwa wadau mbalimbali ndani ya siku 14.





## SEHEMU YA TANO

### URATIBU NA USIMAMIZI

#### 5.1 UTANGULIZI

Uratibu na usimamizi wa shughuli zote za upimaji utafanywa na WyEST kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI. Mafunzo kwa Wathibiti Ubora wa Shule; Maafisa Elimu Msingi wa Halmashauri na Kata; Wakuu wa Shule na Walimu wa madarasa husika, kuhusu upimaji wa mtoto/mwanafunzi yatatolewa kwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

#### 5.2 MAHITAJI NA VITENDEA KAZI

Katika kufanikisha kazi hii, vitendea kazi vitakavyotumika ni pamoja na vifaa vya kuandikia, huduma za kurudufu, vishikwambi, kompyuta, chakula, na usafiri kwa ajili ya washiriki.

#### 5.3 UWASILISHAJI WA TAARIFA NA UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

Huu ni mpango wa Kuboresha Utendaji Shuleni (MKUUS), Wadhibiti ubora wa shule kutoka kila wilaya watakusanya taarifa za Usimu (DPLA) kutoka shule 19. Baada ya kuchambua takwimu za DPLA na kukusanya matokeo,







Ofisi ya Elimu ya Wilaya na Ofisi ya Uthibiti wa Ubora wa Wilaya watakutana kujadili matokeo, waliyojifunza na kubaini marekebisho yanayohitajika, na kisha kuunda/kutengeneza mpango wa ufuatiliaji katika wilaya zao (MKUUS).

Timu ya wilaya (Wadhibiti ubora wa shule wilaya na maafisa taaluma wa wilaya) kwa pamoja watabaini viashiria vitatu ambavyo havikufikia vigezo kutokana na matokeo na kuandaa Mipango ya Uboreshaji ya Wilaya (au kwa Kiswahili: Mpango wa Kuboresha Utendaji wa Shule (MKUUS). Mipango hii inalenga kuipa mikoa na wilaya njia ya wazi ya namna ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wenye kuleta ufanisi kwa kuzingatia masuala yanayoweza kushughulikiwa mara moja katika ngazi ya wilaya. Taarifa za upimaji na MKUUS zitawasilishwa kwa Katibu Mkuu WyEST, na nakala kwa OR - TAMISEMI.

#### **5.4 UFUATILIAJI NA TATHMINI**

Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya upimaji ili kuweka mipango na mikakati endelevu ya kuinua viwango vya utoaji wa elimu nchini kulingana na sheria, sera, kanuni na taratibu zilizopo.



## 5.5 TATHMINI YA VIWANGO VYA UBORA KATIKA ELIMU YA AWALI, DARASA LA I NA II

Tathmini ya ubora wa ujifunzaji katika Elimu ya Awali, Darasa la I na II inazingatia viashiria vya ubora ili kupata matokeo tarajiwa. Alama ya vema ( $\checkmark$ ) itawekwa kwenye kiwango cha ubora stahiki kwa kila kiashiria husika, baada ya Mthibiti Ubora wa Shule (UUS) kukusanya ushahidi wa kutosha kwa kuona ufikiwaji wa kiwango cha ubora wa kiashiria. Hivyo, atakokotoa alama za viwango vya ubora kulingana na Kiunzi cha UUS

### Jedwali Na. 1: Alama za viwango vya ubora kulingana na Kiunzi cha UUS

Viwango vya Ubora	Hairidhishi	Dhaifu	Inaridhisha	Nzuri	Nzuri sana	Bora sana
Alama za viwango vya ubora	0 - 9	10 - 24	25 - 44	45 - 64	65 - 80	81 - 100

Ili kupata alama kwa kila kiashiria kwa kila kigezo, alama ya juu ya kila kiwango cha ubora, imegawanywa kwa idadi ya viashiria vilivyopo. Hivyo, alama za juu kwa kila kiwango cha ubora ni kama ifuatavyo:



## Jedwali Na. 2: Alama za juu za viwango vya ubora kulingana na Kiunzi cha UUS

Viwango vya Ubora	Hairidhishi	Dhaifu	Inaridhisha	Nzuri	Nzuri sana	Bora sana
Alama za juu za viwango vya ubora	9	24	44	64	80	100

Katika kila kigezo, viashiria vyote vina thamani sawa katika kila kiwango cha ubora husika kama inavyoonesha kwenye jedwali lifuatalo:



### Jedwali Na. 3: Thamani ya juu ya viwango vya ubora kwa kila kiashiria

Nyanja	Kigezo	Idadi ya Viashiria	Thamani kwa kila Kiashiria					
			Hairidhishi	Dhaifu	Inaridhisha	Nzuri	Nzuri Sana	Bora Sana
1. Ubora wa Mtaala katika kukidhi mahitaji ya watoto/ wanafunzi	Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali	5	1.8	4.8	8.8	12.8	16.0	20.0
2. Ubora wa Uongozi na Utawala.	Taarifa za kiutawala	4	2.3	6.0	11.0	16.0	20.0	25.0
3. Ubora wa mazingira ya shule na athari zake kwenye ustawi, afya na usalama	Chumba cha Darasa	7	1.3	3.4	6.3	9.1	11.4	14.3



Nyanja	Kigezo	Idadi ya Viashiria	Thamani kwa kila Kiashiria					
			Hairidhishi	Dhaifu	Inaridhisha	Nzuri	Nzuri Sana	Bora Sana
	Samani na vifaa vinavyoendana na umri na mahitaji ya mtoto	1	9.0	24.0	44.0	64.0	80.0	100.0
	Matundu ya vyoo	7	1.3	3.4	6.3	9.1	11.4	14.3
	Mazingira ya kujifunzia nje ya Darasa	8	0.2	0.6	1.1	1.6	2.0	2.5
	Ustawi, afya na usalama wa Mtoto	15	0.6	1.6	2.9	4.3	5.3	6.7
4. Ubora wa mazingira ya shule na athari zake kwenye ustawi, afya na usalama		6	1.5	4.0	7.3	10.7	13.3	16.7



# VIASHIRIA NA VIGEZO - USHIMU (DPLA)

## VIASHIRIA NA VIGEZO

Sehemu hii inaelezea viashiria na vigezo vya upimaji wa matokeo ya mwanafunzi kwa kila kiashiria kama inavyoonesha kwenye jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Viashiria na Vigezo vya Upimaji wa Matokeo ya Mwanafunzi.**

NA.	KIASHIRIA	KIGEZO CHA MAAMUZI
1.	Uwapo wa vifaa na zana za kufundishia	Mwalimu anatumia mwongozo wa kufundishia Darasa la I na II, Mwalimu ameandaa azimio la kazi na andalio la somo
2.	Uwapo wa vifaa vya kujifunzia	Darasa la I na II lina vitabu vya kutosha vya kusoma angalau kwa 80%, na zana za kufundishia na kujifunzia
3.	Mahudhurio ya walimu	Angalau 90% na zaidi ya walimu wamo darasani muda wa kuanza kipindi



NA.	KIASHIRIA	KIGEZO CHA MAAMUZI
4.	Mahudhurio ya wanafunzi	Angalau 90% ya wanafunzi wa Darasa la I na la II lililochaguliwa wamehudhuria shule
5.	Wanafunzi kuwa na madaftari	Angalau 90% ya wanafunzi wa Darasa la I na la II wanayo madaftari ya umahiri wa kusoma
6.	Walimu kupitia na kusahihisha kazi za wanafunzi na kutoa mrejesho	Angalau 80% ya madaftari ya wanafunzi yaliyoangaliwa yamesahihishwa na kuwekwa alama na yana mrejesho wa mwalimu
7.	Maandalizi ya mwalimu ya Ufundishaji	Mwalimu ameandaa azimio la kazi na andalio la somo kwa kufuata muhtasari na mwongozo wa Ufundushaji wa Darasa la I na II
8.	Zoezi la ufundishaji wa umahiri wa kusoma darasani	Mwalimu ameteteleza majukumu 6 kati ya 7 kama yalivyoelekezwa katika kifaa cha shule





NA.	KIASHIRIA	KIGEZO CHA MAAMUZI
9.	Muda wa kufundisha umahiri wa kusoma	Mwalimu alifundisha kwa kutumia dakika 30 kama alivyoandaa katika andalio la somo
10.	Ushirikishi wa mwalimu na wanafunzi	Mwalimu na wanafunzi wametekeleza angalau shughuli 3 kati ya 5 zilizopo katika kifaa cha shule
11.	Mazingira rafiki na salama	Mwalimu ametekeleza angalau shughuli 4 kati ya 5 za mazingira rafiki na salama zilizorodheshwa(rejea zana ya ufuatiliaji wa viwango kipengele cha ustawi, afya, na usalama wa mtoto No. xv)
12.	Elimu Jumuishi	Mwalimu ametekeleza kwa usahihi angalau shughuli 4 kati ya 5 za elimu Jumuishi zilizo rodheshwa
13.	Ufahamu wa herufi	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza kutambua sauti za herufi 8 kati ya 10 kwa ufasaha.







NA.	KIASHIRIA	KIGEZO CHA MAAMUZI
14.	Maneno ya kubuni	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza kutambua maneno ya kubuni 8 kati ya 10 kwa ufasaha
15.	Kusoma kwa ufahamu	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza kujibu maswali angalau 4 kati ya 5 ya ufahamu kutoka katika kifungu cha habari walichosoma
16.	Imla	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza kuandika maneno 8 sahihi kutoka katika sentensi tatu za imla walizosomewa
17.	Utambuzi wa namba	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza kutambua namba 8 au zaidi kwa usahihi kutoka katika maswali 10 waliyopewa
18.	Kujumlisha na kutoa ngazi ya kwanza	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza maswali 8 au zaidi ya kujumlisha na kutoa ngazi ya kwanza kwa usahihi kati ya maswali 10 waliyopewa





NA.	KIASHIRIA	KIGEZO CHA MAAMUZI
19.	Kujumlisha na kutoa ngazi ya pili	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza maswali 5 au zaidi ya kujumlisha na kutoa ngazi ya pili kwa usahihi kati ya maswali 6 waliyopewa
20.	Namba zinazokosekana kwenye mtiririko	Wanafunzi 13 na zaidi wameweza kupata maswali 5 au zaidi kwa usahihi kati ya maswali 6 ya namba zinazokosekana kwenye mtiririko





## MAREJELEO

- Anning, A., & Edwards, A. (2006). *Promoting Children's Learning from Birth to Five: Developing the New Early Years Professional*. UK: McGraw-Hill Education.
- Bar-On, A. (2004). *Early Childhood Care and Education in Africa: The Case of Botswana*. *Journal of Early Childhood Research*. 2(1), 67 - 84.
- Berk, L. E. (2005). *Infants and Children: Prenatal through Middle Childhood* (5th ed.). Boston: Pearson Education Inc.
- Bodrova, E. & Leong, D. J. (2007). *Tools of the Mind: The Vygotskian Approach to Early Childhood Education*. New Jersey: Pearson Prentice Hall. (2nd ed.).
- Hepper, P. (1991). *An Examination of Fetal Learning before and after Birth*. *The Irish Journal of Psychology*, 12(2), 95 - 107.
- Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2013a). *Mwongozo wa Kuandaa na Kutumia Vifaa vya Michezo kwa Watoto Wadogo*. Programu ya Mafunzo Kazini kwa Walezi wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana na Walimu wa Elimu ya Awali. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Utamaduni.





Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (2013b). *Mwongozo wa Utambuzi wa Mapema wa Watoto Wenye Mahitaji Maalumu na Afua Stahiki Umri (0 - 8)*. Programu ya Mafunzo Kazini kwa Walezi wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana na Walimu wa Elimu ya Awali. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Ufundi.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (2014). *Kiunzi cha Uthibiti Uhora wa Shule*. Dar es Salaam: *Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi*. Dar es Salaam: Education Press A.

Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania (TECDEN). (2013). *Kiunzi cha Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania*. Dar es Salaam: TECDEN.

Naudeau, S., Kataoka, N., Valerio, A., Neuman, M. J. & Elder, L. K. (2010). *Investing in young children: An Early Childhood Development Guide for Policy Dialogue and Project Preparation*. Washington: The World Bank.

Paul, A. M. (2010). *Origins: How the Nine Months before Birth Shape the Rest of Our Lives*. New York: Simon and Schuster.





- Selemani, H. (2016). *Malezi na Ujifunzaji Hatua ya I*. Dar es Salaam: Education Press A.
- Selemani, H. (2019). *Malezi na Ujifunzaji Hatua ya II*. Dar es Salaam: Education Press A.
- Taasisi ya Elimu Tanzania. (2016). *Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali*. Dar es Salaam: TET.
- Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Mwongozo wa Mwalimu wa Kufundishia Elimu ya Awali*. Dar es Salaam: TET
- Tanzania Teachers' Union. (2020). *Competence Profile for Early Childhood Education Teachers in Tanzania*. Dodoma: Tanzania Teachers Union.
- The Science of Early Childhood Development. (2007): *National Scientific Council on the Developing Child*. <http://www.developingchild.net>
- UNESCO. (2000). *Education for All: The Dakar Framework for Action*. Dakar, Senegal. Link <http://www.unesco.org/education/efa/ed-for-all/framework.shtml>
- UNESCO. (2007). *EFA Global Monitoring Report: Strong Foundations - Early Childhood Care and Education*. Paris: UNESCO Publishing.
- URT. (2013). *Moduli ya Kwanza: Ujuzi wa Malezi Changamshi kwa Watoto Wadogo*. TET. Dar es Salaam.
- Yelland, N. (Ed.). (2005). *Critical Issues in Early Childhood Education*. Glasgow: Bell.

